USAFIRI

# Huduma za mwendokasi zasitishwa

Na Maulid Mmbaga

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amesema huduma ya mabasi ya mwendokasi katika njia ya Morogoro na Mbagala imesitishwa kwa muda kutokana na uharibifu wa miundombinu uliosababishwa na vurugu za Oktoba 29, mwaka huu.



Hali hiyo ilitokea siku ya Uchaguzi Mkuu wakati wa vurugu na machafuko yaliyosababishwa na vijana waliokuwa wakidai haki za kisiasa na kusababisha uharibifu mkubwa wa mali za umma na binafsi pamoja na vituo vya mabasi.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam, Chalamila (pichani) alisema: "Vituo vingi vya mwendokasi vimeharibiwa na wale wote waliokuwa wakitegemea usafiri huu tunausitisha mara moja. Mfumo wa ukataji tiketi wa mageti pia uliharibiwa.

"Hivyo, tumeagiza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kutoa vibali vya muda mfupi kwa mabasi ya kawaida ili kuendelea kutoa huduma kwa njia zilizokuwa zikitegemewa."

Chalamila aliongeza kuwa hatua hii itasaidia kufanya tathmini ya uharibifu uliotokea na kurudisha huduma katika kiwango kinachokidhi mahitaji ya wananchi.

Alisisitiza kuwa jitihada za pamoja zitaongeza nguvu kidogo ya utoaji huduma katika njia za Morogoro na Mbagala.